# RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi imeundwa chini ya Kanuni ya 106(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2016, na kufafanuliwa katika jadweli la kwanza la Kanuni hiyo. Aidha, Kifungu cha 106(3) cha Kanuni hiyo kimeeleza zaidi kuwa majukumu ya Kamati za kudumu za Baraza yatakua kama yalivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza.

Ripoti za Kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi huwasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 108 (14) ambapo Kanuni hiyo inawajibisha kila Kamati ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa shughuli zake mbele ya Baraza hilo katika Mkutano wa mwezi wa Februari au wakati mwengine wowote ambapo Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza itaamua.

### 1.1 MAJUKUMU YA KAMATI

Majukumu ya msingi kwa mujibu wakanuni za Baraza ambayo kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inapaswa kuyasimamia wakati wa utekelezaji wa kazi zake ni yafuatayo

i. Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.
ii. Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.
iii. Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.
iv. Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Seriklali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.
v. Kuchambua mapendekezo ya Seriklali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.
vi. Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.
vii. Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.
viii. Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa

## 1.2 OFISI ZINAZOSIMAMIWA NA KAMATI

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika utekelezaji wa kazi zake imekuwa ikizisimamia Ofisi zifuatazo:

i. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, na
ii. Ofisi ya Rais, na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

## 1.3 UTARATIBU NA MIZUNGUKO YA KAZI ZA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA, 2017/2018

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viogozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ilifanya kazi zake katika mizunguko mitatu, ikiwa ni jumla ya wiki sita, ambazo zilifanyiwa kazi kama ifuatavyo:

1. Kamati ilifanya kazi zake Unguja kuanzia tarehe 14/08/20 17 hadi tarehe 25/08/2017 kwa mzunguko wa kwanza.
2. Kuanzia tarehe, 13/11/2017 hadi tarehe 17/11/2017, Kamati ilifanya kazi zake Unguja na tarehe20/11/2017 hadi 24/11/2017, Kamati ilimalizia kazi zake kwa Upande wa Pemba kwa mzunguko wa pili.
3. Aidha Kamati ilifanya kazi zake Unguja kuanzia tarehe 15/01/2017 hadi 26/01/2017 kwa mzunguko wa tatu.

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika utekelezaji wa kazi zake katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imeweza kupokea taarifa za utekelezaji kutoka Ofisi zote mbili.

## 1.4 MUUNDO WA KAMATI

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mheshimiwa Omar Seif Abeid | Mwenyekiti |
| 2. | Mheshimiwa Panya Ali Abdallah | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mheshimiwa Amina Iddi Mabrouk | Mjumbe |
| 4. | Mheshimiwa Hussein Ibrahim Makungu | Mjumbe |
| 5. | Mheshimiwa Mussa Ali Mussa | Mjumbe |
| 6. | Mheshimiwa Mtumwa Suleiman Makame | Mjumbe |
| 7. | Mheshimiwa Ame Haji Ali | Mjumbe |

Aidha, Kamati inaratibiwana Makatibu wawili ambao ni:

1. Ndugu Karima Abdul Wahab
2. Ndugu Talib Enzi Talib

# SEHEMU YA PILI

## OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

### 2.0 OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS IMEUNDWA NA IDARA NA TAASISI ZIFUATAZO:

i. Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti Madawa ya Kulevya
ii. Tume ya Uchaguzi Zanzibar
iii. Wakala wa Seriklali wa Uchapaji Zanzibar.
iv. Idara ya Kukabiliana na Maafa
v. Tume ya UKIMWI
vi. Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ
vii. Idara ya Watu wenye Ulemavu
viii. Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa
ix. Baraza la Wawakilishi
x. Idara ya Huduma za Makamu wa Pili wa Rais
xi. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
xii. Idara ya Mipango Sera na Utafi
xiii. Ofisi kuu Pemba.

### 2.1 TUME YA KITAIFA YA URATIBU NA UDHIBITI DAWA ZA KULEVYA

Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti wa dawa za kulevya ina jukumu kuu la kuratibu mapambano dhidi yauangamizaji, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya. Pia inajukumu la kutoa taaluma kwa jamii juu ya athari za dawa za kulevya, tiba pamoja na ushauri nasaha kwa waathirika wa dawa hizo.

Kwa mwakawa fedha 2017/2018, Tume imeweza kutekeleza majukumu yake ya kazi kwa ufanisi mkubwa licha ya kwamba Tume hiyo inachangamoto kadhaa zinazokabiliana nazo ambazo kwa kiasi kikubwa imekuwa ikirejesha nyuma mapambano dhidi ya mtandao huo wa biashara hiyo haramu ya madawa ya kulevya. Pamoja na juhudi kubwa inayochukuliwa na Seriklali kupitia Tume hiiambapo miongoni mwa majukumu ambayo kamati imependezwa nayo ni pamoja na:

i. Kuendesha mikutano ya uhamasishaji wa mradi kwa walengwa, wakiwemo viongozi wa dini ,masheha na viongozi katika ngazi mbalimbali;
ii. Kuratibu uaanzishaji wa mtandao wa vijana wenye kutumia dawa za kulevya;
iii. Kuendesha mafunzo maalum kwa watunga sera na wasimamizi wa utoaji huduma za UKIMWI kwa watumiaji wa dawa za kulevya na kupunguza madhara;
iv. Kufanya utafiti kwa vijana katika ya umri wa miaka 14-25 kwa ajili ya kufuatilia tabia za watumiaji wa dawa za kulevya.

v. Kusimamia kikamilifu Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia (TREATMENT AND REHABILITATION CENTER) kiliopoKidimini Wilaya ya Kati Unguja na kwamba kituo kipo katika hatua ya umalizaji wa majengo saidizi ambayo ni jiko, sehemu ya kulia na sehemu ya kufulia nguo.

Pamoja na mambo ambayo Kamati imependezwa nayo, lakini bado kuna baadhi ya changamoto ambazo Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya inakabiliana nazo.

**Changamoto:**

1. Upotevu wa vielelezo vya kesi za madawa ya kulevya katika baadhi ya kesi zinazowakabili watuhumiwa wa madawa ya kulevya.

2. Kukosekana kwa takwimu halisi juu ya idadi ya vijana walioingia na kutoka katika *Sober Houses*.

3. Kukosekana kuzifikia mara mara familia za vijana walio athirika na madawa ya kulevya na waliopata nafuu pamoja na kukosa kupatiwa mafunzo juu ya njia bora ya kuwanusuru vijana hao kutorudia tena utumiaji wa madawa ya kulevya.

4. Kukosa kushirikishwa kwa shirika la umma la utangazaji la *ZBC* katika utoaji wa vipindi vya elimu kuhusu athari za madawa ya kulevya kwa kuzingatia kwamba chombo hicho cha Seriklali kinawafikia wananchi waliowengi.

5. Kukosekana kwa takwimu na taarifa juu Skuli zilizopatiwa elimu kuhusu madawa ya kulevya ili kufamu kiwango cha idadi ya skuli zilizofikiwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18.

6. Kuuosekanana kupatiwa taaluma ya ujasiriamali vijana walioatirika na madawa ya kulevya, ili wawe na shughuli za kufanya na waondokane na fikra za kureje katika utumiaji wa Dawa hizo.

7. Kukosa kushirikishwa watu wanaoishi karibu na maeneo ya madiko katika bandari zisizo rasmi ili kusaidia katika upatikanaji wa taarifa za uhalifu na uingizaji na utumiaji wa dawa za kulevya.

8. Kutoshirikishwa kikamilifu Wakuu wa Mikoa katika kupata taarifa ili kudhibiti madawa ya kulevya nchini.

### 2.1.1 Maoni /Ushauri/Maagizo Ya Kamati:

i. Pamoja na hatua zinazoendelea katika ujenzi wa kituo cha kidimni Kamati inataka kujua tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo na kujua thamani halisi ya ujenzi huo toka kuanza hadi kukamilikakwake na nii gharama zake kiasi gani.

ii. Kamati imeshauri shirika la utangazaji la ZBC kupitia ZBC T.V na ZBC Redio kushirikishwa kikamilifu katika utoaji wa vipindi vya elimu kuhusu athari za madawa ya kulevya kwa kuzingatia kwamba chombo hicho ni cha Seriklali ambacho kinawafikia wananchi waliowengi.

iii. Kamati imeagiza Tume kutoa takwimuna taarifa juu skuli zilizopatiwa elimu kuhusu madawa ya kulevya ili kufahamu kiwango na idadi ya skuli zilizofikiwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 na wanafunzi wangapi waliofikiwa na taaluma hii na kwamba kazi ya kutoa taarifa hii kwa umma iwe endelevu.

iv. Kamati imeishauriTume kuzifikia mara kwa mara familia za vijana walio athirika na madawa ya kulevya na waliopata nafuu kupitia SoberHouse na kuwapatia mafunzo na njia bora ya kuwanusuru vijana hao kutorudia tena kwenye utumiaji wa madawa ya kulevya.

v. Kamati imeiagiza Tume kutoa taarifa na takwimu katika mwezi wa June juu ya idadi ya vijana walioingia na kutoka katika Sober House ili jamii ifahamu kazi zinazofanywa na Tume hiyo.

vi. Kamati imeagiza Tume kuhakikisha kuwa inawapatia vijana wanaoacha Dawa za kulevya Taaluma ya ujasiriamali ili wawe na shughuli za kufanyapindi wanapotoka kwenye Sober House ili waondokane na fikra za kutokurejea tena katika utumiaji wa Dawa za kulevya.

vii. Kamati inaagiza suala la kuwashirikisha zaidi watu wanaoishi karibu na maeneoya madiko katika bandari zisizo rasmi ili kusaidia katika upatikanaji wa taarifa za uhalifu na uingizaji wa dawa za kulevya katika maeneo ya madiko yao.

viii. Kamati imeshauri Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya kuwa karibu na taasisi zote zinazosimamia kesi za madawa ya kulevya ili kuhakikisha kwamba tatizo la upotevu wa vielelezo vya kesi za madawa ya kulevya halitokei tena kama hapo mwanzo ambapo kamati ilibaini kasoro hizo kujitokeza kwenye baadhi ya kesi zinazowakabili watuhumiwa wa madawa ya kulevya.

ix. Kamati imeagiza Tume ya Kuratibu na kudhibiti Dawa za Kulevya kuwashirikisha kikamilifu Wakuu wa Mikoa na Wilaya na masheha na

mabalozi wa nyumba kumi katika kupata taarifa ili kudhibiti madawa ya kulevya nchini.

x. Kamati imeagiza Tume kushirikiana na Taasisi husika kuhakikisha mazingira bora ya ulinzi Bandarini yanaimarishwa ikiwa ni pamoja na kuweka wataalamu na vifaa vya kutosha ili kudhibiti uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya kupitia Bandari rasmi.

xi. Kamati imeagiza Tume kuhakikisha kuwa eneo lililopangwa kwa ajili ya uanzishwaji wa miundombinu mbali mbali katika mradi wa ujezi wa kituo cha kurekebisha tabia kiliopo Kidimni, linafanyiwa usafi kwa kuondoa msitu uliopo katika eneo hilo.

## 2.2 TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR

Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imeundwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kifungu 119(1). Majukumu ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, yameelezwa katika Katiba ya Zanzibar 1984, Sheria ya Ofisi ya Tume ya Uchaguzi, 2017, Sheria ya Kura ya Maoni ya 2010 pamoja na Sheria nyenginezo. Majukumu hayo ni pamoja na:

i. Usimamizi wa jumla wa mienendo ya Uchaguzi wa Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Viongozi wa Seriklali za Mitaa (Madiwani).

ii. Kufanya uchunguzi wa idadi, mipaka na majina ya Majimbo ya Uchaguzi ya Zanzibar.

iii. Uandikishaji wa wapiga kura na Uendelezaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

iv. Kukuza na Kuratibu Elimu ya Wapiga Kura.

v. Kusimamia na kuendesha Kura ya Maoni.

### 2.2.1 Changamoto:

i. Kamati imebaini tatizo ambalo bado lipo la upungufu wa ghala la kuhifadhia vifaa pamoja na kwamba Seriklali imeshawapatia nyumba ambayo ilikua ikimilikiwa na Shirika la Bandari.

ii. Matatizo ya vyombo vya usafiri hasa magari ambapo kamati imebaini kwamba Tume ya Uchaguzi imepeleka maombi wizara ya fedha kupatiwa fedha za ununuzi wa magari mawili mapya pamoja na kwamba magari kumi na sita yalipelekwa karakana kuu ya Seriklali na kufanyiwa matengenezo pamoja na kwamba magari hayo kwa sasa yanafanya kazi lakini bado tatizo la usafiri kwa magari hasa kwa wafanyakazi bado haitoshelezi.

iii. Kamati imebaini tatizo laukosefu wa majengo ya ofisi za kudumu za wilaya.

iv. Pamojana mambo mengine kamati imebaini tatizo la upungufu wa wafanyakazi ingawaje kamati ilielezwa kwamba kibali cha uajiri tayari kimeshatolewa na Seriklali lakini hadi leo bado hawajaajiriwa.

**2.2.2 Ushauri na Maagizo ya Kamati:**

i. Kamati imeshauriofisi za Tume Uchaguzi za wilaya zipatiwe majengo yao wenyewe ili yaweze kutumika kwa ofisi za kudumu za wilaya.

ii. Kamati imeshaurikufanyiwa haraka mchakato wa ununuzi wa magari mawili mapya ambayo Tume iliombaWizara ya fedha kupatiwa fedha ambazo inaaminika kwamba wizara ya fedha imeshatoa asilimia hamsini.

iii. Kamati imeagiza kufanyiwa haraka ukarabati wa jengo la Tume walilo kabidhiwa na Seriklalihivi karibuni liliopo mkabala na Tume ya Uchaguzi ili jengo hilo liweze kutumika kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vya tume ambavyo vimehifadhiwa kwenye jengo la ghala ya CCM liliopo kikwajuni.

iv. Kamati pia inashauri wizara kusimamia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ndogoya tume ya uchaguzi iliopo Pemba kwa mwaka fedha 2017/18.

## 2.3 WAKALA WA SERIKLALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR

Wakala wa Seriklali wa Uchapaji Zanzibar ni miongoni mwa Taasisi za Seriklali zilizopo chini ya wizara ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais zinazosimamiwa na Kamati ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.Katika Mwaka wa fedha wa 2017/18.kamati inapongeza jitihada za wakala katika kukitangaza kiwada cha uchapaji ndani na nje ya nchi ili kuweza kupokea kazi na kuweza kukiendesha kiwanda hicho kwani ni kiwanda ambacho kimesheheni mitambo mikubwa yenye kutumia techologia ya kisasa.

Aidha wakala wa uchapaji yupo katika hatua ya kukitanua kiwanda ili huduma zake ziwafikie wananchi wote wa Unguja na Pemba , pia wakala imeanza hatua za kuanzisha bohari kwa ajili ya uuzaji na kutoa huduma ya vifaa vya kuandikia na mahitaji mengine kwa taasisi za Seriklali na watu binafsi hatua ambayo itachangia kukua kwa soko lake na kuongezeka wa mapato ya Wakala Wa Seriklali wa Uchapaji Zanzibar hata hivyo pamoja na mambo mazuri yanayoanza kujitokeza lakini kumekuwepo na baadhi ya changamoto ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi ili kiwanda hicho kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisimkubwa zaidi.

### 2.3.1 Changamoto:

Katika utekelezaji wakazi zake za kawaida, kamati imebaini changamoto kadhaa inazokabiliana na taasisi hiyo kama ifuatavyo.

i. Taasisi nyingi za Seriklali bado hazijaikikia wito uliotolewa na Seriklali wa kuzitaka taasisi hizo kupeleka kazi zao za machapisho kwenye kiwanda hicho kama ambavyo Seriklali imekuwa ikiziagiza wizara hizo kila mara.

ii. Uhaba wa soko la kwa ajili ya kazi za wakala na kwamba ni asilimia 40 tu ya kiwango cha kazi zinazopatikana na Wakala kutoka nje.

iii. Ukosefu wa jengo la kudumu la Wakala Pemba pamoja na ghala la kuhifadhia bidhaa za zinazozalishwa kiwandani hapo kwa upande wa Pemba.

iv. Ukosefu wa wafanyakazi wenye taaluma ya biashara kwa wafanyakazi wa wakala wa kiwanda cha mpiga chapa mkuu wa Seriklali ambao wataweza kuuza bidhaa zinazozalishwa kiwandani hapo.

### 2.3.2 Ushauri/Maagizo:

i. Kamati inashauri kuharakishwa uajiri wa wafanyakazi wataalamu wenye taaluma ya biashara kwa Ofisi ya Wakala wa Seriklali.

ii. Kamati imeagiza Wakala kuendelea kutafuta soko la nje pamoja na kwamba kuna mazungumzo ya kibiashara yaliowahi kufanyika kati ya Wakala na Shirika la magazeti la Tanzania Bara TSN ili kuongeza mapato katika taasisi hiyo ili iweze kufikia lengo.

iii. Kamati imeagiza kuharakishwa kwa ujenzi wa Bohari ya Wakala ili kuweza kutoa huduma za uuzaji wa vifaa vyao (stationaries) kwa taasisi za Seriklali na binafsi.

iv. Kamatiimeshauri Seriklali kuweka msisitizo zaidi kwa wizara na taasisi zote za Seriklali sambamba na kuzishajihisha sekta binafsi kupeleka kazi zao zote kiwandani hapo jambo ambalo litawezesha kiwanda hicho kuzalisha zaidi na kupata mapato yatakayowezesha kiwanda hicho kuleta tija iliyotarajiwa kinyume na hivi sasa ambapo imegundulika kwamba bado kuna baadhi ya wizara na idara za Seriklali bado hawajakubali kupeleka kazi zao hapo jambo ambalo ni kwenda kinyume na maagizo ya Seriklali.

v. Kamati imeunga mkono lile agizo la Muheshimiwa Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba wizara ya Fedha ikate fedha za OC ili kulipia deni kwa baadhi ya wizara zenye madeni ya kiwandani hapo.

vi. Kamati imemuagiza Wakala wa Seriklali wa Uchapishaji kuchukua juhudi za kumaliza hatua za kukodi jengo na kulifanyia ukarabati kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa za Wakala Pemba.

vii. Kamati imeiagiza Wakala wa Seriklali kukamilisha mikataba ya ushirikiano wa kibiashara kati yake na shirika la magazeti ya Seriklali Tanzania bara (TNS) ili kukuza soko la nje.

## 2.4 KAMISHENI YA KUKABILIANA NA MAAFA

Kamisheni ya kukabiliana na maafa ni taasisi iliyoundwa kwa lengo la kuiwezesha jamii ya Wazanzibari kuwa na uhimili wa kuweza kukabiliana na maafa kabla na baada ya kutokea kwa dhamira ya kupunguza athari za maafa hayo. Kwa mwaka wa fedha 2017/18 Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa imepanga kujenga uelewakwa jamii katika kukabiliana na maafa kwa kuratibu shughuli zake ikiwa ni kutoa mafunzo kwa jamii, kuwahudumia waathirika wa majanga ya maafa pamoja na kutoa miongozo inayosimamia utekelezaji washughuliza maafa.

### 2.4.2 Changamoto:

Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa katika utekelezaji wa kazi zake imekuwa inakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo:

i. Inategemea fedha za Maendeleo kutoka kwa wahisani ambako kunapelekea shughuli zilizopangwa kutokamilika kwa wakati.

ii. Ufinyu wa Bajeti na kupelekea kuacha kutekeleza shughuli nyengine muhimu.

iii. Ukosefu wa jengo la ofisi ambapo kwa sasa Kamisheni inatumia jengo la Kituo cha huduma za dharura.

iv. Kuchelewa kupata voti ambayo itapelekea Kamisheni kuweza kujitegeme kama Sheria ya kukabiliana na maafa inavyelekeza

Hata hivyo, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kuiongeea Bajeti Kamisheni ya kukabiliana na Maafa ili iweze kusimamia kwa ufanisi suala la maafa yanapotokezea.Aidha kamati inapongeza Ofisi ya Makamu wa Pli wa Rais kwa kuweza kuanzisha Akauti Maalum kwa ajili ya kupokea michango ya kukabiliana na maafa yanapotokea.

### 2.4.3 Ushauri/Maagizo Ya Kamati

i. Kamati inaishauri Wizara licha kwamba Kamisheni inachukua juhudi za kuwahifadhi wahanga pale maafa yanapotokezea lakini Kamisheni kuwa na maeneo maalumu yaliyotengwa kwa ajili ya wahanga wa maafa sambamba na kuweko maghala mahsusi ya kuhifadhia vifaa hivyo vinavyotumika kwa maafa yanapotokea.

ii. Kamati imeiagiza Kamisheni kuharakisha kuandaa muundo pamoja na Kanuni ya Sheria Nam. 1 ya Kupunguza na Kukabiliana na Maafa ya mwaka 2015.ili Taasisi hiyo iweze kufanyia kazi kwa ufanisi.

iii. Kamati imeishauri Kamisheni kuhakikisha kuwa inavitunza kwa kuvihifadhi vizuri vifaa vyote vilivyonunuliwa kwa ajili ya kazi za kukabiliana na maafa ili vifaa hivyo viweze kusaidia katika nyakati tofauti wakati yanapotokea maafa.

iv. Kamati imeiagiza Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa kwa kushirikiana na Idara ya Uvuvi kufanya utafiti ili kuweza kugundua tatizo linalosababisha kufariki au kupata ulemavu wa maisha kwa wavuvi wanaotumia gesi katika shughuli zao za uvuvi.

## 2.5 IDARA YA WATU WENYE ULEMAVU

Idara ya Watu wenye Ulemavu ni miongoni mwa Idara zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais(OMPR). Katika mwaka wa fedha wa Bajeti ya 2017/2018, Idara ilipanga kusimamia programu nne (4) kuu nazo ni;- Ujumuishwaji, Kuimarisha huduma za Ofisi, Uwezeshaji wa Watu wenye Ulemavu, Kukuza uelewa wa jamii juu ya Watu wenye Ulemavu na kutekeleza maagizo ya Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu ili kuhakikisha haki na fursa sawa kwa Watu wenye Ulemavu zinapatikana.

Katika Idara ya Watu Wenye Ulemavu kamati katika kutekeleza kazi zake ilibaini baadhi ya changamoto ambazo zinaikabili Idara hiyo pamoja na ukweli kwamba Seriklali inafanya juhudi kubwa ya kupambana nazo ili kuzitatua au kuzimaliza kabisa.

### 2.5.2 Changamoto:

i. Uhaba wa bajeti kwa Idara ya watu wenye ulemavu ni moja kati ya mambo ambayo yanachangia kutokamilika kwa kazi zao na kutofikia malengo waliojipangia.

ii. Kuwepo kwa uhaba wa vyombo vya usafiri; Idara imekuwa na tatizo la kuwa na vyombo vya usafiri kwa ajili ya kazi za Idara za kila siku ukizingatia kwamba shughuli za idara hii zinahitaji ufuatiliaji wa mara kwa

mara kama vile kufuatilia kesi katika mahakama mbali mbali, lakini pia kuwafuatilia waathirika mbali mbali wanaofanyiwa vitendo vya udhalilishaji. Kwa sasa Idara ina gari moja tu ambayo inatumika na mkurugenzi, na vespa mbili ambazo kwa ujumla hazikidhi mahitaji.

iii. Kesi za udhalilishaji za Idara ya watu wenye ulemavu kukosa kufika katika ngazi za kisheria za maamuzi na utoaji haki kutokana na kutokuwa na nguvu za kutosha kwa watendaji wanaofuatilia kesi hizo.

iv. Kukosekana kwa Mkalimani wa lugha za alama jambo ambalo limekuwa linachangia kukosekana kwa mawasiliano miongoni mwa baadhi ya waathirika

### 2.5.3 Ushauri/Maagizo Ya Kamati

i. Kamati imeishauri Wizara kuiangalia sana Idara ya Watu wenye Ulemavu kuwaongezea Bajeti itakayosaidia kukidhi mahitaji na utekelezaji wa majukumu yake.

ii. Kamati imeishauri Wizara kutoa kipaumbele maalumu katika Bajeti ya Seriklali kwa ajili ya ajira kwa watu wenye ulemavu.

iii. Kamati imeishauri Wizara kuona umuhimu wa kuliwekea Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu Kasma yake badala ya Baraza hilo kuendelea kutegemea Bajeti ya Idara ambayo bado haijitoshelezi.

iv. Kamati imeishauri Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu ifanye utafiti kuelewa Takwimu za idadi ya Walimu wenye taaluma za watu wenye mahitaji maalum ili waweze kusaidia kuwaendeleza kielimu watu wenye mahitaji maalum.

v. Kamati imeishauri Idara ya Watu wenye ulemavu katika Bajeti yake kuzingatia na kuweka kipaumbele ufatiliaji wa matokeo ya malalamiko dhidi ya udhalilishaji wa watu wenye ulemavu, ziara za kimafunzo pamoja na madhimisho ya Watu wenye ulemavu kitaifa.

vi. Kamati imeishauri Idara ya Watu wenye ulemavu kuanzisha Jumiya na waratibu wa Watu wenye ulemavu katika majimbo na Shehia jambo ambalo litairahisishia Idara kuwezakuwatambua mara moja watu wenye ulemavu.

vii. Kamati imeiagiza Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais kuipatia Idara ya Watu wenye ulemavu usafiri wa gari na Dereva kwa ajili ya watendaji ili waweze kutekeleza majukumu yao ya kazi ikiwemo ufuatiliaji wa kesi za udhalilishaji za watu wenye ulemavu ikizingatiwa kwamba Idara kwa muda

mrefu imekuwa na Dereva mmoja ambaye hatoshelezi kwa shughuli za Idara nzima.

viii. Kamati imeiagiza Idara ya Watu Wenye Ulemavu kuhakikisha kuwa inasimamia vikundi vya ujasiriamali vya watu wenye ulemaavu ili viweze kupata usajili na mitaji ya kujieneleza kiuchumi.

ix. Kamati imeiagiza Wizara kuhakikisha kuwa inafuatilia kesi za udhalilishaji watu wenye ulemavu na kutoa taarifa za mwenendo wa kesi hizo kila baada ya miezi mitatu.

x. Kaamati imeiagiza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuhakikisha kuwa inasimamia ipasavyo uzingatiaji wa kufuata muongozo wa kuweka Miundombinu rafiki itayokidhi mahitaji ya watu wenye Ulemavu katika majengo ya zamani na mapya yanayoendelea kujengwa na Taasisi Binafsi na za Seriklali.

## 2.6 BARAZA LA WAWAKILISHI

Baraza la Wawakilishi ni taasisi inayojitegema ambayo inatekeleza programu kuu mbili:

i. Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Seriklali.
Programu hii inajukumu la kuhakikisha haki na utawala wa Sheria unatekelezwa.

ii. Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi.
Programu hii inakusudia kuweka mazingira mazuri ya kazi pamoja na kuwajengea uwezo wajumbe na wafanyakazi wa Baraza.

### 2.6.1 Changamoto:

i. Kuwepo kwa mrejeo wa sauti (eco) katika ukumbi wa mikutano ya Baraza la jambo ambalo hupelekea baadhi ya wakati wajumbe na wasikilizaji vikao kushindwa kusikia vizuri mijadala ya vikao hivyo.

### 2.6.2Ushauri/Maagizo ya Kamati

i. Kuhusu suala la jengo la Baraza la Wawakilishi, Kamati imeshauri lifanyiwe matengenezo hasa katika Ukumbi mkubwa wa mikutano ili kuondoa mrejeo wa sauti (ECO) jambo ambalo limekuwa likizungumziwa kwa muda mrefu sasa.

ii. Pia Kamati imeagiza Ofisi ya Baraza kushughulikia haraka suala la kuimarisha mazingira ya kazi katika ofisi zake ikiwa ni pamoja na kununua vipoza hewa (A/C) pamoja na masuala ya maslahi kwa wafanyakazi wa Baraza, ili kuimarisha mazingira mazuriya kazi zao.

iii. Kamati imeagiza Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kufuatilia kwa karibu sana suala la upatikanaji wa hati ya umiliki wa kiwanja chake kilichopo nyamanzi pamoja na kuandaa utaratibu wa kulihifadhi eneo hilo na eneo la kiwanja cha Baraza la Wawakilishi kilichopo Pemba .

## 2.7 IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ, SMT NA MUUNGANO

Kamati ilipata fursa ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Idara ya uratibu. Kwa ujumla kamati imeridhishwa na uteketelezaji wa kazi za idara hiyo. Kamati pamoja na mambo mengine iliweza kufanya ziara mbali mbali kuangalia maendeleo na changamoto ya miradi ya **TASAF III,** Unguja Pemba na Tanzania Bara.

Kamati imefarajika sana kuona Seriklali kupitia mfuko wa maendeleo wa jamii (TASAF) unaowasaidia wananchi katika nyanja tofauti za huduma za jamii kama vile maji, elimu, afya, mazingira na masuala mengineyo.

Kamati ilitembelea miradi tofauti kuangalia utekelezaji na maendeleo ya miradi hiyo.Miongoni mwa miradi iliyotembelewa kwa Unguja na Pemba ni; Mradi wa kutoa ajira za muda kwa kaya maskini katika bwawa la kuhifadhi maji ya kilimo cha umwagiliaji na ulishaji wa wanyama uliopo Mtende Makunduchi, Mradi wa kujengatuta la kuzuia maji ya chumvi kuingia katika maeneo ya kilimo cha maji katika bonde la Mbagani Ndagoni-Pemba, Mradi wakutoa ajira za muda wakupanda Miti ya mivinje kwa ajili ya shughuli za ujenzi katika Shehia ya Mwange na Mradi wa ujenzi wa Skuli ya Sekondari katika Shehia ya Potoa.

Aidha; Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea na kukagua baadhi ya Miradi ya **TASAF** inayosimamiwa na **TASAF** Makao Makuu huko Dar Es Salam, pamoja na kupata mafunzo juu ya masuala mbali mbali ya uendeshaji wa Mradi yakiwemo Utaratibu wa ulipaji fedha kwa walengwa kwa njia ya kielektroniki (E-Payment ), Taratibu za ukaguzi wa Mradi, pamoja na Mfumo wa ulalamikaji. Kamati ilitembelea Mkoa wa Pwani ,Wilaya ya Kibaha na kupokea taarifa ya utekelezaji wa Mradi wa **TASAF** pamoja na kukagua baadhi ya miradi ikiwemo Mradi wa Bwawa,Mradi wa Shamba darasa la kilimo cha muhogo, Mradi wa barabara na Mradi wa kuweka na kuwekeza iliyopo katika kijiji cha Vikude. Lengo la ziara hiyo ni ilikuwa ni kujifunza, kubadilishana uzoefu pamoja na kuona changamoto na mafanikio katika Mradi wa **TASAF111** ambao unatekelezwa kwa pamoja Zanzibar na Tanzania Bara.

Kwa ujumla kamati imeridhishwa na utekelezaji wa kazi za Idara. Idara inafanya vizuri katika kuhakikisha majukumu yake yanatekelezwa ipasavyo. Katika Idara hii, Kamati iliangalia suala la miradi ya TASAF, fedha za mfuko wa jimbo, na masuala ya Muungano.Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa na Ofisi kwa mafanikio makubwa ni mradi wa **TASAF III.**

### 2.7.1 Changamoto Za Usimamizi wa Miradi ya TASAF

i. Baadhi ya masheha wanapostaafu kushindwa kurejesha vifaa vya uendelezaji wa Miradi.

ii. Kutokuwepo kwa taarifa za walengwa wa miradi wanapohama katika maeneo yao yaliyoanzishwa miradi.

iii. Kukosekana usimamizi bora na kuendelezwa kwa miradi ya Tasaf inapokamilika kwa sekta zinazohusika na miradi hiyo.

iv. Kamati imebaini kuwepo kwa malalamiko ya udanganyifu kwa baadhi ya maafisa hasa kwa malipo ya mtandao E-payment hasa kwa watu wasiojua kusoma kwenye mpango wa majaribio hasa kwa njia ya E-payment.

v. Uwepo wa kaya maskini ambazo hazijafikiwa na mpango kutokana na upungufu wa rasilimali fedha.

### 2.7.2 Maoni /Ushauri/Maagizo ya Kamati:

i. Kamati inahimiza Seriklali kuhakikisha kuwa inatoa mchango wake kwa Mradi hiyo ya TASAF kwa wakati kwani kutofanya hivyo kutapelekea kuzorotesha utekelezaji na ufanisi wa Mradi kwa walengwa.

ii. Kamati inaagiza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuhimiza sekta husika juu ya umuhimu wa usimamiaji na uendelezaji wa miradi iliyokamilika ili iweze kuleta tija zaidi kwa kaya maskini zilizolengwa.

iii. Kamati imeshauri Idara ya Uratibu kuwasimamia wataalamu wa miradi ya TASAF juu ya utowaji wa elimu kuhusu miradi husika ili walengwa waweze kutumia utaalamu huo kwa kuitunza na kuiendeleza miradi hiyo kwa manufaa yao kwa ujumla.

iv. Kamati inaishauri kununua mipira ya maji na kuweka kwenye mambwawa ya kuhifadhia maji ili kusaidia kuyahifadhi na kuwarahisishia wanakaya upatikanaji wa huduma ya maji kwa urahisiili kuwezesha kuyatumia katika shughuli zao za kila siku.

v. Kamati imeshauri idara ya uratibu wa shughuli za SMZ (TASAF) wakati wa kuibuliwa Miradi ya skuli na wanakaya ni vyema zaidi ujenzi wa skuli hizo uwe wa ghorofa ili kwenda sambamba na uhaba wa ardhi iliyopo sambamba na kukidhi mahitaji ya skuli kwa wanakaya hao.

vi. Kamati imeshauri kuwepo utaratibu wa wazi juu utolewaji wa taarifa ya uwanzishwaji wa miradi ya tasaf katika majimbo.

vii. Kamati imeagiza Waratibu na Wakurugezi wa miradi ya TASAF kuhakikisha kuwa wanasimamia upatikanaji wa taarifa za ukaguzi wa miradi husika ya TASAF, ili kupatikana kwa ripoti ambayo itawezesha kuelewa mafanikio na changamoto za miradi

viii. Kamati imeagiza idara ya uratibu wa shughuli za SMZ (TASAF) kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuweka akiba kwa vikundi vya ujasiriamali kwa wanakaya wa miradi ya TASAF.

ix. Kamati inashauri Seriklali ione umuhimu wa kuwapatia Wawakilishi wote fedha za mfuko wa jimbo japo kwa viwango tofauti kwani wote ni viongozi na wana wajibu wa kuwatumikia wananchi wote.

**2.8 OFISI YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ- DAR-ES-SALAAM.**

Ofisi ya uratibu wa shughuli za SMZ – Dar-es-Salaam ni miongoni mwa ofisi zilizopo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo majukumu yake ya msingi ni kuratibu shughuli zaSMZ kwa upande wa Tanzania Bara.Miongoni mwa majukumu ya ofisi ni kuimarisha ushirikiano katika taasisi/Wizara za SMZ na zile za Muungano, kukuza na kuimarisha mashirikiano na washirikawa maendeleo, na taasisi za kibalozi.

Kamati katika mzunguko wake ilipata fursa ya kutembelea ofisi hiyo na ilibaini baadhi ya changamoto ambazo wanakabiliana nazo.

**2.8.1 Changamoto:**

i. Uchakavu wa jengo. Licha ya maboresho makubwa sana yaliyofanywa katika baadhi ya maeneo ya jengo ambapo kwa ujumla wake jengo hilo haliendani na hali halisi ya ofisi yenyewe.

ii. Uhaba wa ofisi katika jengo. Kwa mfano Jengo la Ofisi ya Uratibu Dar-es-Salam limekuwa likitumika kwa ajili ya Ofisi ya Uratibu vile vile kwa ajili ya ofisi za studio na chumba cha habari cha ofisi za ZBC.

iii. Posho la mazingira magumu linalotolewa hivi sasa halikidhi haja hasa ukilinganisha na hali halisi ya maisha ya Dar Es Salam, kwa wafanyakazi wanaotoka Zanzibar.

iv. Viongoziwa baadhi ya wizara za SMZ kutokuripoti ofisini hapo wakati wakiwepo kikazi Dar es salam jambo ambalo linasababisha ofisi kukosa kujua taarifa muhimu ambazo ofisi hii inapaswa kuzifahamu.

**2.8.2 Ushauri na Maagizo ya Kamati:**

i. Licha ya kufanyika kwa baadhi ya ukarabati katika baadhi ya sehemu ya jengo la ofisi, kamati inashauri ukarabati zaidi unahitajika ukizingatia upakaji rangi wa jengo, ili liweze kuleta haiba na taswira nzuri ya Seriklali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakati Seriklali imo mbioni kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo ambapo nia ya Seriklali ni kulijenga jengo jengine ambalo litakuwa na hadhi inayolingana na uhalisia wa ofisi yenyewe.

ii. Ukizingatia kwamba ofisi hii ndio ofisi pekee ya SMZ kwa upande wa Tanzania bara**,** Kamati imeishauri Ofisi ya Makamu wa Pili kutekeleza mpango wake wa kuharakisha mpango wake wa ujenzi wa jengo bora na la kisasa litakalotumika kwa ajili ya Idara ya Uratibu wa shughuli za SMZ na taasisi nyengine zilizokusudiwa.

iii. Kamati imeiagiza Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ iliyopo Dar es Salaam kutafuta utaratibu zaidiwa kuweza kuitangaza Ofisi hiyo kupitia maadhimisho ya ya sherehe ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kila mwaka ili taasisi mbali mbali za Seriklali ya SMT, SMZ, balozi na za binafsi ziweze kuitumia ofisi hiyo na kurahisisha shughuli za ushirikiano kati ya taasisi hizo na Seriklali.

iv. Kamati inaishauri Seriklali kuu kufuatilia suala la upatikanaji wa share ya tozo la kusanyo ya malipo ya minara ya kimataifa ya kuongozea meli la zaidi ya shilingi bilioni 1ili iweze kupata mapato yake. Ofisi ya Uratibu ya SMZ iliyopo Dar es Salam imetekeleza wajibu wake wa kuratibu ufuatiliaji lakini bado suala hilo lipo katika mivutano kati ya taasisikuu za Seriklali mbili za smz na smt zinazohusika. Ni karibu kipindi cha miaka miwili sasa Zanzibar imekuwa ikidai deni hilo la asilimia 41 za mgao wote ambapo Tanzania Bara linapata asilimia 59.

v. Kamati imeiagizaWizara husika kutoa muongozo maalum kwa wizara na taasisi za Seriklali juu ya umuhimu wa kuitumia ofisi ya uratibu wa shughuli za SMZ iliyopo dar es salaam.

vi. Kamati inaishauri ofisi kuendelea kuwapatia mafunzo watendaji wake yanayoendana na majukumu na hadhi ya Ofisi, ukizingatia umuhimu Ofisi hii kwani Viongozi mbali mbali ikiwa ni pamoja na Mabalozi na Viongozi wakuu wa Nchi za nje na wanaofanyia mikutano kwenye ofisi hiyo.

vii. Kamati inaishauri ofisi ishirikiane na Idara ya Diaspora Zanzibar katika kuratibu masuala mabli mbali yanayohusu Diaspora Dar-es-Salam.

viii. Kamati inaishauri ofisi kuendeleza utaratibu wa kuanzisha program za mafunzo ya UKIMWI kwa maafisa wake ili kutekeleza mpango wa Seriklali wa kukabiliana na janga hilo kwa watendaji wake.

## 2.9 IDARA YA SHEREHE NA MAADHIMISHO YA KITAIFA

Miongoni mwa majukumu iliokabidhiwa Idara ya sherehe na maadhimisho ya kitaifani kuratibu na kusimamia sherehe na Maadhimisho ya kitaifa pamoja na kusimamia shughuli za kuwaenzi Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Idara imeendelea kutekeleza kazi zake kwa ufanisi na kwa namna ya pekee, kamati inatoa pongezi kwa Mhe Balozi Seif Ali Iddi ambaye ndie Mwenyekiti wa kamati ya Kitaifa ya Sherehe kwa kufanikisha maadhimisho ya kutimiza miaka 54 ya Sherehe za Mapinduzi kwa mwaka 2018 ambayo yalifanywa kwa namna ya kipekee.

Pamoja na kufanikiwa kwa sherehe hizi vizuri bado kuna changamoto ambazo Idara inakabiliananazo.

### 2.9.1 Changamoto:

i. Ufinyu wa Bajeti; idara inakabiliwa na bajeti ndogo kuweza kuhudumia shughuli zake za kila siku pamoja na kuratibu shughuli za sherehe mbali mbali za kitaifa.

ii. Uhaba na uchakavu wa vifaa,kama mashamiana yanayotumika katika sherehe za kitaifa.

### 2.9.2 Ushauri na Maagizo ya Kamati:

i. Kamati imeagiza kutafuta namna ya kupata fedha kwa ajili ya kununua vifaa vipya na vya kisasa ambavyo vitatumika katika shughuli na Sherehe mbali mbali za kitaifa, na pia kufanyia biashara kwa kukodisha kwa ajili ya kuingiza mapato Seriklalini.

## 2.10 TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

Tume ya UKIMWI Zanzibar ni Taasisi iliyoundwa kwa Sheria Nambari 3 ya mwaka 2002 ya Seriklali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tume ni Taasisi inayojitegemea chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Katika utekelezaji wa majukumu yake Tume inakabiliwa na baadhi ya changamoto, ambazo zinawapelekea kutofanyakazi zao kwa ufanisi zaidi.

### 2.10.1Changamoto:

i. Uhaba wa watoa huduma za afya na wafanyakazi, nafasi ndogo za maeneo ya kutoa huduma, uchache wa vifaa tiba na vifaa vya uchunguzi bado ni changamoto katika utoaji wa huduma za afya ya uzazi hasa katika utoaji wa huduma za saratani ya kizazi.

ii. Kutojitokeza vya kutosha kwa vijana wa kike katika huduma ukilinganisha na vijana wa kiume.

iii. Kasi ndogo ya Mabadiliko ya tabia katika jamii.

### 2.10.2Ushauri/Maagizo/Mapendekezo:

i. Kamati imeishauri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutokana na uzito wa usimamiaji wa suala la UKIMWI ni vyema Ofisi kuipatia kasma yake ya kibajeti Tume ya UKIMWI, ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

ii. Kamati imeishauri Tume kuendelea kusimamia uzingatiaji wa masuala ya UKIMWI katika sekta za Seriklali na zile za binafsi kama Sheria na miongozo ya Nchi ikiwemo Sera, Mkakati na Sheria ya VVU na UKIMWI na miongozo inayohusiana na Usalama na Afya sehemu za kazi inavyoelekeza.

iii. Kamati inaagiza kuharakisha utayarishaji wa mfuko wa VVU na UKIMWI, ili kusaidia kugharamia utekelezaji wa majukumu ya Tume na mipango mbali mbali ya VVU na UKIMWI ikiwemo ile ya wadau ili kuwe na uendelevu wa programu hizo.

iv. Kamati imeiagiza Tume kuhakikisha kuwa inaimarisha jitihada za ufuatiliaji wa taarifa za maambukizi ya UKIMWI katika ngazi ya Shehia na hata balozi wa nyumba kumi ili kuweza kubaini watu wanaoishi na VVU ili kuweza kupatikana takwimu sahihi zisizogongana na maeneo mengine ya ufuatiliaji.

v. Kamati inaishauri Tume iendelee kuihamasisha jamii kufanya uchunguzi wa saratani ya kizazi mara kwa mara hasa kwa watu wanaoishi na VVU ambao wamo katika hatari ya kupata saratani hiyo kutokana na kuwa na VVU.

vi. Kamati inaishauri Tume kuhakikisha kuwa inasimamia uhamasishaji wa mabadiliko ya tabia katika jamii ili kuweza kujikinga na maambukizo ya UKIMWI.

vii. Kamati inaishauri Tume kuweka mikakati maalum kwa ajili ya kuwafikia vijana wa kike na kuwapa mafunzo kuhusu hali ya maambukizi ya UKIMWI kwa vijana hao.

## 2.11 OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS – PEMBA

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 **OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS – PEMBA**inaendelea kutekeleza lengo la kuratibu shughuli za Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi.

### 2.11.1 Changamoto

i. Ufinyu wa nafasi za kufanyia kazi kwa wafanyakazi wa OMPR.

ii. Kukosekana kwa nyumba sahihi ya kudumu kwa ajili ya kufikia Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais anapofanya ziara zake kisiwani Pemba.

iii. Ukosefu wa wafanyakazi wenye taaluma ya biashara kwa Ofisi ya Wakala wa Seriklali wa Uchapaji.

### 2.11.2 Ushauri/ Maagizo Ya Kamati

i. Kamati imeishauri OMPR Pemba kuzingatia shauri la Ofisi ya Makamu wa Pili Pemba la ujengaji wa jengo la ziada ambalo litakidhi mahitaji ya Ofisi hiyo.

ii. Kamati imeishauri Seriklali kuipatia Ofisi ya Makamu Wa Pili wa Rais Pemba jengo linalotumiwa na ORKSUUU Bora mara tu itakapohama ili kuzipatia nafasi taasisi zake zilizo chini ya wizara hiyo ambazo zina changamoto ya makaazi ambazo ni Tume ya Kitaifa Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Wakala wa Seriklali wa Uchapaji na Idara ya Watu Wenye Ulemavu.

iii. Kamati imeihimiza OMPR kuharakisha kufuatilia na kukamilika kwa taratibu za kuanza kwa ujenzi wa nyumba ya makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais iliyopo Pagali Wilaya ya Chake Chake ili ujenzi huo uweze kufanyika kwa wakati na kumuwezesha kiongozi huyo kuwa na sehemu maalum ya kufikia akiwa kisiwani Pemba.

iv. Kamati imeshauri Wakala wa Seriklali wa Uchapaji kujenga miundo mbinu bora katika Ofisi zake za Pemba ili kuiwezesha taasisi hiyo kufanya kazi kibiashara na Seriklali kupata mapato zaidi katika eneo hilo.

**OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI**

## 2.12 MUUNDO WA OFISI

**Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inaundwa na Idara na Taasisi zifuatazo:**

i. Ofisi ya Faragha ya Rais;
ii. Ofisi ya Baraza la Mapinduzi;
iii. Idara ya Huduma za Rais.
iv. Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu;
v. Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi;
vi. Idara yaUendeshaji na Utumishi;
vii. Idara ya Mipango Sera na Utafiti;
viii. Ofisi ya Usalama wa Seriklali;
ix. Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba.

## 2.13 OFISI YA FARAGHA YA RAIS

Ofisi ya faragha ina majukumu ya kuratibu na kusimamia shughuli za Mh.Rais pamoja na kufuatilia utekelezaji wa ahadi zake kwa lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma zilizo bora na kuweka ukaribu baina ya wananchi na Seriklali yao hasa na kiongozi wao mkuu ambaye ni Mh.Rais.

Kwa mwaka wa fedha 2017/18 ofisi imeendelea kutelekeza majukumu yake kama ilivyojipangia. Kimsingi Kamati imeridhishwa sana na utendaji wa ofisi ya faragha kwa kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa ahadi za Mh.Rais pamoaja na kuhakikisha shughuli zote za ofisi hiyo zinatekelezwa kama zilivyopangwa licha ya kuwepo kwa changamoto wanazokabiliana nazo.

### 2.13.1 Changamoto:

i. Kuwepo kwa athari kubwa za mong’onyoko wa ardhi karibu katika nyumba zote za Ikulu. Kwa mfano; nyumba ya Ikulu Migombani, Kibweni, Bwefum na Mkokotoni kwa Unguja na Mkoani- Pemba.

### 2.13.2 Ushauri/Maagizo:

i. Kamati imeshauri Seriklali kuu kuanzisha mradi maalumu utakaosaidia katika kukabiliana na athari kubwa za mong’onyoko wa ardhi uliopo karibu katika nyumba zote za Ikulu. Kwa mfano; nyumba ya Ikulu Migombani, Kibweni, Bwefum na Mkokotoni kwa Unguja na Mkoani- Pemba.

ii. Kamati inaiagiza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhakikisaha kuwa ujenzi wa ukuta katika Ikulu ya Mkoani unaendelezwa kwa hatua za awali huku kukitafutwa njia bora mbadala za kitaalamu ili kunusuru jengo la Ikulu kutokana na hali ya mmong'onyoko unaoendelea.

## 2.14 OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

Ofisi ya Baraza la Mapinduzi ambayo ni moja katika ofisi muhimu sana katika ofisi Taasisi za ofisi ya Rais, Ofisi hii inajukumu kuu la kuandaa vikao vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake ikiwa ni pamoja na Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu.

Katika mwaka wa fedha wa 2017/18, imepanga kutekeleza program mbili zifuatazo nazo ni:
**Programu ya usimamizi ya majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu.**

Lengo la program hii ni kuhakikisha uwajibikaji wa Seriklali katika kutoa huduma kwa wananchi.
**Programu ya pili ni ya utumishi na uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.**Lengo la programu ni kuimarisha mazingira ya kazi, mahusiano ya umma na kuongeza ujuzi wa wafanyakazi.

### 2.14.1 Ushauri na Magizo ya Kamati

i. Kamati inaiagiza Wizara kuhakikisha kuwa inatafuta eneo jengine litakalotumika kwa ajili ya Ofisi za Baraza la Mapinduzi ambapo kwa hatua za awali ofisi zilizopo zifanyiwe ukarabati na kutiwa rangi ili ziendelee kutumika hadi zitakapopatikana ofisi nyengine.

ii. Kuhusu ukumbi wa Mikutano wa Makatibu wakuu ,Kamati inaishauri Seriklali bila ya kuathiri na kuzingatia taratibu za kimataifa za Urithi na Uhifadhi wa mji mkongwe kupata kibali ili kuweza kuupanua ukumbi huo uwe na nafasi kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za watendaji hao wakuu wa Seriklali.

iii. Kwa upande mwengine Kamati inashauri Seriklali iwapo ufumbuzi wa kupata kibali cha UNESCO kutafuta namna mbadala ili ORMBM ipatiwe eneo jengine ambalo litaweza kujengwa ukumbi huo.

iv. Kamati inashauri umuhimu wa kuharakishwa kuendeleza mkakati wa kuanzishwa maktaba katika Afisi ya Baraza la Mapinduzi ambayo itakuwa ya kielektroniki "E-Library" ili kuwawezesha viongozi wakuu na waheshimiwawengine kutumia huduma hizo katika muda na mahala popote.

## 2.15 IDARA YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA URATIBU WA WAZANZIBARI WANAOISHI NJE YA NCHI

Idara hii ina dhamana ya kuhakikisha Zanzibar inanufaika na uhusiano uliopo baina yake na jumuiya za kikanda na kimataifa. Aidha Idara inawaunganisha wazanzibari walionje ya nchi na nchi kwa dhamira ya kuwaweka karibu na kujuwa maendeleo ya nchi yao na waweze kusaidia katika nyanja mbali mbali za maisha ya watu ikiwa ni pamoja na shughuli za kiuchumi na kijamii.

### 2.15.2 Changamoto :

i. Idara inakabiliana na changamoto ya kuchelewa kupata taarifa za vikao vya mashiriano baina ya Zanzibar na Tanzania bara.

### 2.15.3Ushauri/Maagizo/ Mapendekezo:

i. Kamati imeshauri idara ya diaspora kuhakikisha kwamba fursa za kiuchumi na kibiashara zitokanazo na wanadaspora wa Tanzania zinasimamiwa na kuendelezwa vizuri kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Kwa mfano uwekezaji wa hospital za watoto na uwanzishwaji wa kiwanda cha samaki, na mradi wa ujenzi wa nyumba za kuishi.

ii. Kamati imeishauri idara kuwashajihisha wanadispora wa kanda kujikusanya pamoja ili wajione kama wanadispora wengine na kuweza kutoa michango yao mikubwa katika fursa za kiuchumi na kibiashara.

iii. Kamati imeishauri idara kuwa na mfumo wa takwimu (data base) wa utoaji wa taarifa ili iweze iweze kuwafikia na kuwatambua kiurahisi wanadiaspora wa kikanda

iv. Kamati imeagiza idara kutanua wigo kwa kuwatumia wanadiaspora wa Zanzibar kutangaza utalii ili kukuza maendeleo ya kiuchumi.

v. Kamati imeshauri Seriklali kuu itafute namna ya kuiwezesha idara ya diaspora kufanya utafiti wa kuwatambua wanadaspora wa Zanzibar waliopo mashariki ya mbali.

## 2.16 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Idara hii inajukumu la kuratibu na kusimamia Sheria, Kanuni za Utumishi na Kusimamia Shughuli za Uendeshaji wa Ofisi; Idara kimuundo Idara imeunda sehemu kuu tatu nazo ni Kitengo cha Utumishi, Kitengo cha Uendeshaji, Kitengo cha Utunzaji wa Kumbukumbu.
Vilevile Idara inaratibu na kusimamia kazi za Kitengo cha Manunuzi, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Kitengo cha Sheria na Kitengo cha Uhasibu.

### 2.16.1Ushauri/Maagizo/ Mapendekezo:

i. Kamati imeagiza idara kuhakikisha kuwa inaandaa utaratibu endelevu wa kupima afya ya wafanyakazi baada ya kila kipindi cha miezi sita na kamati ipatiwe taarifa ya zoezi hilo.

ii. Kamati iemeagiza idara kuharakisha kuandaa programu ya kutoa taaluma ya ufahamu juu ya maradhi yasiyo ambukiza kwa watumishi ili waweze kupata uelewa juu ya afya zao.

iii. Kamati imeshauri idara kufanya mapitio ya mahitaji ya mafunzo na kuandaa mpango wa mafunzo ya watumishi.

iv. Kamati imeagiza kuandaa watendaji wa ofisi wa ngazi za chini ili endapo mkuu wa ofisi amefikia muda wa kustaafu kusikuwepo na changamoto ya nafasi hiyo.

## 2.17 IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI

Idara ya Mipango Sera na Utafiti ni miongoni mwa Idara/Ofisi nane zilizo chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Jukumu kuu la Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ni kuratibu utekelezaji wa shughuli za Mipango, Sera na Tafiti za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

### 2.17.1 USHAURI/MAAGIZO

i. Kamati imeishauri Idara kuhakikisha kuwa kunakuwa na matokeo ya utafiti kwa wananchi juu ya fursa za masoko katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

ii. Kamati imeishauri Idara kutoa taarifa za Mpango wa kupunguza Umasiki nchini (MKUZA) ili jamii iweze kuuelewa mpango huo na kuondokana na umasikini.

iii. Kamati imeagiza Wizara kuharakisha kuandaa Programu ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa ili kusaidia udhibiti wa mmong’onyoko katika majengo ya Ikulu za Mheshiwa rais hasa Pemba.

iv. Kamati imeishari Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kuimarisha mashirikiano na vyuo vikuu katika masula ya utafiti.

### 2.17.3 KITENGO CHA SERA, UFUATILIAJI NA TATHMINI

Seriklali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba imedhamiria kuimarisha utendaji kazi kwa viongozi na watendaaji wake ili, pamoja na mambo mengine, iweze kutoa huduma bora kwa wananchi na kuwaletea maendeleo endelevu. Hivyo, pamoja na hatua nyengine muhimu ilizozichukua, imeamua kuanzisha kitengo maalum cha ufuatiliaji na tathmini katika Ofisi ya Baraza la Mapinduzi ili kifanye tathmini ya kina ya utendaji na uwajibakaji katika kutekeleza majukumu mbali mbali ya kazi kwenye taasisi za umma.

Kitengo cha Sera, Ufuatiliaji na Tathmini kimeanzishwa kwa madhumuni ya kupata taarifa muhimu za utekelezaji wa mipango, mikakati na Sera za Seriklali kwa lengo la kujua na kujipima ufanisi wa shughuli zilizotekelezwa na kupima jinsi raslimali fedha zinazotolewa endapo zimetumika ipasavyo na kama zimetoa matokeo mazuri yaliyokusudiwa.

### 2.17.5 CHANGAMOTO ZA KITENGO

i. Kutokamilika kwa Muundo maalum wa Kitengo.

ii. Kitengo kutokuwa na wafanyakazi wakutosha na wanaohitajika

### 2.17.6 USHAURI/MAAGIZO YA KAMATI

i. Kamati imeiagiza Wizara kuhakikisha kuwa katika Bajeti ya 2018/2019 Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathminikinapangiwa Kasma yake ili kiweze kuwa na nguvu katika ufuatiliaji na kutathmini maendeleo ya mipango mbali mbali ya Seriklali.

ii. Kamati imeishauri Wizara kusimamia uharakishwaji wa uandaaji wa Muundo husika waKitengo cha Sera, Ufuatiliaji na Tathmini kabla ya Bajeti 2018/2019 ili Kitengo hicho kiweze kufanyakazi kwa mujibu wa utaratibu.

iii. Kamati imeiagiza Wizara kuhakikisha kuwa Kitengo cha Sera na Ufatiliaji na Tathmini kinatoa Ripoti ya utekelezaji wa kazi zake katika kipindi cha awamu ya mwisho ya kazi za Kamati ya kusimamia Ofisi za viongozi Wakuu wa kitaifa.

iv. Kamati imeiagiza Wizara kuhakikisha kuwa Kitengo kinaajiri watendaji wenye uwezo na uzoefu ili waweze kufanyakazi kwa ufanisi.

v. Kamati imekiagiza Kitengo cha kutathmini kulifanyia tathmini Shirika la Bandari na kutoa ripoti kuhusu utendaji wa shirika hilo.

## 2.18 IDARA YA USALAMA WA SERIKLALI (GSO)

Idara ya Usalama wa Seriklali ni idara muhimu katika Seriklali na ndio yenye jukumu la kusimamia masuala yote ya usalama wa Seriklali kwa ujumla wake, Kamati katika utekelezaji wa kazi zake imepata nafasi ya kutembelea Idara hii na kuangalia utendaji wa kazi zake za kila siku. kwa ujumla Kamati imeridhishwa na utendaji wa idara hii. Pamoja na kazi kubwa na nzuri zinazo fanywa na idara hiyo ya GSO bado zipo baadhi ya changamoto ambazo idara hiyo inakabiliana nazo kama vile

**i.** Upungufu wa bajeti kwa Idara hiyo ambayo Kamati imelibaini kuwa ni jambo ambalo linasababishia Idara hiyo kushindwa kufikia malengo ya kazi zake ambazo imejipangia.

**ii.** Uchakavu wa jengo linalitumiwa na Idara hiyo pamoja na kwamba Seriklali ipo mbioni kuwatafutia sehemu mbadala kama ambavyo kamati ililiona na kulishauri kutokana na ufinyu wa sehemu yenyewe.

**iii.** Upungufu wa vitendea kazi Kamati imebaini kwamba kuna mapungufu ya baadhi ya vifaa ambavyo ni muhimu vinavyohitajika katika kutekeleza vyema kazi zao.

**iv.** Kamati imebaini kwamba ipo haja ya kuwa na eneo maalumu lenye usalama kwa ajili ya kuhifadhia nyaraka muhimu za Idara na Seriklali kwa ujumla.

### 2.18.2 Ushauri na Maagizo ya Kamati:

**i.** Kamati inashauri kufanywa marekebisho zaidi katika ofisi ya GSO ili kuondokana na hali ya uchakavu wa jengo na kuwawezesha wafanyakazi kufanyakazi katika mazingira bora, mazuri na yenye usalama zaidi.

ii. Kamati imeagiza idara GSO kutoa taarifa za wafanyakazi ambao wanatakakuajiriwa katika Wizara ya Afya na tayari wameshafuata taratibu zote za ukaguzi lakini mpaka hivi sasa Idara ya GSO haijatoa taarifa yeyote kuhusu ukaguzi huo.

iii. Kamati inahimiza wizarakulifanyia ukarabati jengo La Ofisi za Idara za GSO ili liweze kuwa na hali nzuri sambamba na kuangalia uwezekano wa kupatikana kwa jengo jengine litakalotumika kwa ajili ya Ofisi za Idara hiyo ambalo litalingana na hadhi ya Idara husika na litakalokidhi vigezo vya usalama vya wafanyakazi pamoja na usalama wa nyaraka za Seriklali.

iv. Kamati imeshauri kufanyiwa marekebisho Sheria inayohusiana na uwepo wa Idara ya Usalama wa Seriklali (GSO)-Zanzibar, ambayo kimsingi ni moja ya sababu ya kuwepo kwa changamoto nyenginezo.

## 2.19 IDARA YA MAWASILIANO IKULU

Idara ya Mawasiliano Ikulu ni miongoni mwa Idara zinazounda Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Lengo la Idara hii ni kusimamia shughuli za Mheshimiwa Rais na kuimarisha mawasilinao Ikulu.

### 2.19.1Ushauri na Maagizo ya Kamati:

i. Kamati imeshauri Idara kuandaa utaratibu na kupanga muda muafaka wa kurusha vipindi vya redio na televisheni vya hotuba ya Mheshimiwa Rais ili wananchi waweze kusikiliza hotuba zake kwani jambo hili litasaidia sana wananchi kuzijua habari za mambo yanayotekelezwa na Rais wetu kwa lengo la kuwapatia habari hasa wananchi wanaoishi vijijini.

## 2.20 OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI – PEMBA

Ofisi imepanga kutekeleza majukumu yake ya kibajeti kwa mwaka wa fedha 2017/18 kupitia Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia shughuli za ORMBLM – Pemba pamoja na Miradi ya Maendeleo.

### 2.20.1 Changamoto:

i. Kuendelea kuwepo kwa mmong’onyoko katika Ikulu ya Mkoani.

ii. Kuachwa kwa muda mrefu kuendelezwa kwa ujenzi wa ukuta wa Ikulu ya Mkoani ambao utasaidia katika kuzuia mmong’onyoko katika eneo hilo.

### 2.20.2 Ushauri /Maagizo ya Kamati:

i. Kamati imeiagiza Wizara kuhakikisha kuwa inaipatia Ofisi ya faragha gari ili iweze kuondokana na tatizo la usafiri.

ii. Kamati imebaini kuwa licha ya kuwepo juhudi za awali za kuanzisha ujenzi wa ukuta wa mawe kusaidia kuzuia hali ya mmong’oko katika Ikulu ya Mkoani, bado hali hiyo si nzuri na inaendelea kuleta athari. Hali hiyo imetokana na kuachwa kwa muda mrefu kuendelezwa kwa ujenzi wa ukuta huo ambapo jumla ya shilingi milioni thelathini zimetolewa kwa Wizara ya Miundombinu kwa ajili ya kusimamia ujenzi huo. Hivyo Kamati inaiagiza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhakikisaha kuwa ujenzi wa ukuta huo unaendelezwa huku kukitafutwa njia mbadala za kitaalamu ili kunusuru jengo la Ikulu na hali ya mmong’onyoko unaoendelea.

iii. Kamati imeridhika na hali ya maendeleo ya mradi wa ujenzi wa nyumba ya Ikulu ya Micheweni ambapo imeshauri ujenzi kuendelezwa kwa wakati na mategemeo ya Kamati baada ya ujenzi kukamilika liwe ni jengo lenye ubora litakalolingana na hadhi ya makaazi ya kiongozi wa kitaifa.

# SEHEMU YA TATU

## HITIMISHO

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa ujumla imeweza kufanikisha jukumu lake la msingi la kuisimamia Seriklali kupitia Wizara hizi mbili kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Kamati imeweza kufanya kazi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na taasisi zake zote kwa kadri ilivyoona inafaa kwa kuzingatia muda na umuhimu wa majukumu ya taasisi hizo. Kamati ilifuatilia na kuyafanyia kazi maeneo yaliyopewa kipaumbele katika utekelezaji wa bajeti ya Seriklali ya mwaka 2017/18 katika wizarazote mbili inazozisimamiwa na kamati yetu ambapo wizara hizi zimekidhi viwango vya utendaji kazi wake kama ambavyo ilianishwa katika hotuba ya bajeti ya wizara hizo.
.
Aidha; Kamati inatoa pongezi za dhati kwa viongozi wote wa Ofisi zilizo chini ya Kamati kuanzia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya ili kuhakikisha kuwa nchi yetu inaendelea kuwepo katika hali ya amani na utulivu na pia kamati inampongeza Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, Mawaziri wa Ofisi zote mbili, Naibu Waziri, Makatibu wakuu Manaibu Katibu Wakuu,Wakurugenzi pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri wanazoendelea kufanya katika kuwatumikia wananchi.

Mwisho Kamati inapenda kutoa shukurani kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid kwa ushauri, miongozo na maelekezo mbali mbali katika kutekeleza kazi za Kamati kwa ufanisi mkubwa. Aidha Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo na kuiwezesha Kamatiyetu kufanya kazi zake vizuri.